**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA IBADA YA KUWEKWA WAKFU MAPADRE SITA (6), MAKERE- KIGOMA.

**TAREHE 28 JULAI 2022**

- ***Mhashamu Baba Askofu Joseph Mlola, Askofu wa Jimbo Katoliki la Kigoma;***
- ***Wahashamu Maaskofu wote mliopo;***
- ***Waheshimiwa sana Mapadre wapya;***
- ***Waheshimiwa sana Mapadre, Mashemasi na Watawa wote mliopo;***
- ***Waheshimiwa Viongozi wote wa Madhehebu mengine ya Dini;***
- ***Mheshimiwa Kamishna Thobias Andengenye, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na viongozi wote wa Serikali mliopo;***
- ***Waheshimiwa Wabunge mliopo;***
- ***Waamini wa Parokia ya Makere na Jimbo Katoliki la Kigoma;***
- ***Wageni waalikwa, wananchi wote mliohudhuria ibada hii takatifu, mabibi na mabwana.***

**TUMSIFU YESU KRISTO! KRISTO! *IMANA ISHIMWE!***

Ndugu zangu ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia fursa ya kushiriki ibada hii takatifu siku ya leo. Mimi binafsi ninayo furaha kubwa kujumuika nanyi leo kupokea baraka hii kubwa ya ndugu zetu hawa sita kufikia daraja takatifu la Upadre. Ni jambo kubwa sana na la kumshukuru Mungu kwa wema wake na rehema zake hizi nyingi. Naomba mpokee salaam nyingi za upendo kutoka kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Anawasalimia sana na anawapongeza kwa baraka hii kubwa ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia kwa pamoja. Mheshimiwa Rais alitamani sana kuwepo hapa nanyi leo, lakini kwa sababu zilizo nje ya uwezo wake hakuweza. Hivyo amenituma nimuwakilishe na nifikishe pongezi zake za dhati kwa Mapadre hawa wapya na kwenu nyote. Anasema amefurahia kupatikana kwa mapadre wapya sita kwa mara moja ambao watatuongoza kuutafuta ufalme wa mbinguni kwa kuishi maadili mema ya sala, upendo na kazi.

Nami naomba niungane na Mheshimiwa Rais kuwapongeza kwa dhati Mapadre hawa wapya na kwa kipekee Jimbo Katoliki la Kigoma na waamini wote. Vilevile ninawapongeza wazazi na walezi wa mapadre hawa wapya kwa maana ninaamini wametimiza maandiko yasemayo: ***"mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha hata atakapokuwa mzee" (Mithali 22:6)***. Pia nawapongeza walimu wa Seminari zote mlizopitia, kwa mifano na mafunzo mema na miongozo ambayo imetupatia fursa ya kukutana hapa kwenye ibada hii takatifu ya kuwapokea katika daraja takatifu la upadri. Wote kwa pamoja hongereni sana.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa na Waamini wenzangu***

Katika somo la Elimu ya Biblia (*Bible Knowledge*) nililosoma zamani, tulifundishwa kwamba: viongozi wa jumuiya za kwanza za Kikristo waliitwa 'Wazee' au 'Maaskofu'. Kwa kuwekewa mikono walichaguliwa na mitume kuwa mawakili wao. Huwa na nguvu na karama ya Mungu. Huitwa pia wasimamizi au wachungaji. Wateule hao hawakushughulikia tu mahitaji ya jumuiya bali walifundisha pia. Mapadre wa leo ndio waliochukua madaraka ya 'Wazee' na 'Maaskofu' wa nyakati za mitume. Sasa ninaposimama mbele yenu katika siku hii njema, ninakumbuka maneno yaliyoandikwa katika Waraka wa **1 Timotheo 3:1** ambayo yanasema ***"Ni neno la kuaminiwa, mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema"***. Ndugu zangu Mapadri wetu wapya mmepata kazi njema, yenye wito mkuu na baraka kuu nyingi. Hongereni sana maana sisi wengine tulishindwa! Na wana-Makere, waliozaa mrembo anayeitwa Mbonimpaye mlichangia kushindwa kwangu kuwa Padre! Lakini naomba pia niwakumbushe waheshimiwa Mapadre wapya jambo moja, japo najua mnalijua vizuri sana. Katika kazi njema mliyoipata, maandiko yanasema ***"basi imempasa Askofu awe mtu asiyelaumika, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji na ajuaye kufundisha"*** (***1 Timotheo 3:2)***. Katika wito wenu huu mkuu, sisi walei tunatamani milango yenu iwe ni maeneo ya kimbilio na hata wengine wenye shida mbalimbali, tukavutwe nanyi na tumuone Kristo katika nyuso zenu, nasi tukapate faraja ya Kristo na amani ya Mungu Baba yetu kupitia kwenu. Mkatufundishe kuwa na kiasi na kuwa na busara kubwa itakayoponya na kuokoa roho zetu. Katika kazi yenu ya ukuhani tusipate sababu ya kuwalaumu wala kuwashitaki ninyi kwa namna yeyote kama inavyoelekezwa katika ***Kitabu cha Tito 1:7 "Maana imempasa Askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa Mungu; asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake, asiwe mwepesi wa hasira, asiwe mlevi wala mgomvi, asiwe mpenda mapato ya aibu"***.

***Ndugu zangu waamini wenzangu***

Mungu wetu mwema kwa mara nyingine tena ametupatia baraka hii ya watumishi wanyenyekevu ambao watatutumikia sisi kama kanisa katika maisha yao yote. Kwa namna ya pekee watafanya kazi njema ya utume kwa niaba yetu, kazi ambayo sisi nasi tulipaswa kuifanya. Lakini wao wamejitoa kwa unyenyekevu mkubwa na kujiweka wakfu. Kwa sababu hiyo Mungu ametupa wajibu wa kufanya. Ametuagiza tumtolee zaka na sadaka. Katika kitabu cha ***Mambo ya Walawi 27:30 anasema zaka zote ni mali yake na tena ni takatifu kwake, na zaka yote hiyo akawapatia Walawi hawa kuwa sehemu ya urithi wao kama ilivyoandikwa katika Kitabu cha Hesabu 18:21***, **maana wamejitoa wakfu kwake kwa ajili yetu na hawana urithi katika nyumba zetu.** Hivyo, ndugu zangu waamini, tunatenda dhambi kwa Mungu tusipotoa zaka na sadaka zetu ili kuwategemeza watumishi hawa wa Mungu,

kwa sababu kwa kufanya hivyo tunamuibia Mungu zaka yake ambayo amesema ni takatifu na akawapa urithi watumishi wa nyumba yake. Tunapoacha kutoa kwa moyo wa shukrani kwa Mungu, na watumishi wake wakapata taabu, tunajitafutia laana na kukimbiza baraka majumbani mwetu na kwenye maisha yetu ya kila siku.

***Ndugu zangu wana Makere na Watanzania kwa ujumla***

Kwa kumalizia salamu za Serikali naomba niseme mambo matatu:

(i) **Jambo la kwanza,** Uharibifu wa mazingira limekuwa tatizo kubwa na lenye athari mbaya sana kwetu kama Taifa na kwa dunia nzima. Uharibifu wa mazingira umetusababishia upungufu na wakati mwingine ukosefu kabisa wa mvua katika maeneo yetu. Kwa mfano mwaka huu, katika baadhi ya mikoa mvua imekuwa ndogo sana na hivyo kupelekea mavuno yasiyoridhisha. Hivyo, nawaasa sana tutunze mazingira yetu, tulinde misitu inayotuzunguka na tuache tabia ya kuchoma moto hovyo kwa faida yetu wenyewe na vizazi vijavyo. Serikali haitamvumila mtu yeyote ambaye atabainika kuharibu mazingira kwa sababu mtu huyo ni adui wa maendeleo na ustawi wetu. Mtu anayekaribisha njaa katika jamii yetu kwa kuharibu misitu na vyanzo vya maji hawezi kuwa rafiki yetu! Hata katika Biblia Takatifu tumeagizwa tuilime hii bustani nzuri na kuitunza **(Mwanzo 2:15)**. Viongozi wangu wa dini nawaomba kwa unyenyekevu, mtusaidie kuendelea kuhubiri juu ya umuhimu wa kutunza mazingira mazuri tuliyobarikiwa na Mungu wetu. Kama Wahashamu Maaskofu mlivyofundisha wakati wa mkutano wa AMECEA uliomalizika hivi karibuni. Maana hata uharibifu wa mazingira hamfurahishi Mungu, na ni dhambi vilevile.

(ii) **Jambo la pili**, ambalo ningependa kusisitiza ni kuhusu elimu. Maandiko yanasema ***"Mkamate sana elimu, wala usimwache aende zake; mshike, maana yeye ni uzima wako" (Mithali 4:13)***. Ndugu zangu, tunapowanyima watoto wetu elimu maandiko yanasema tunawanyima uzima maana huo ni uzima wao. Bila kusoma na kuelimika Waheshimiwa Mapadre wetu hawa wapya, leo hii tusingelikuwa hapa katika ibada hii takatifu. Tukitaka kubadilisha maisha yetu na ya familia zetu tuwapatie elimu watoto wetu na kuwasisitiza waishike hasa. Wazazi wasio peleka watoto wao shule wanawakosea watoto wao wenyewe, wanamkosea Mungu wao na wanaikosea Serikali yao. Ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba, licha ya Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kutusaidia kupeleka watoto wetu shule kwa kuondoa ada mpaka kidato cha sita sisi bado hatupeleki watoto wetu shule. Kwa hili pia nawaomba sana viongozi wetu wa dini waendelee kulikemea na kuwasihi waamini wazingatie elimu kwa watoto wao, maana kwa kutokufanya hivyo wanamkosea Mungu wao na wanatenda dhambi.

(iii) **Na jambo la Tatu,** ambalo ningependa kuwakumbusha ni kwamba, Mwezi Agosti mwaka huu mnamo tarehe 23 tutakuwa na zoezi muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu na sisi wenyewe binafsi. Zoezi hilo ni la Sensa ya watu na makazi. Ninawaomba sana ndugu zangu tujitokeze kushiriki zoezi hilo na kuhesabiwa. Takwimu zitakazopatikana katika zoezi hili zitaisaidia Serikali kuweka mikakati bora na sahihi ya kuwafikishia maendeleo na mahitaji muhimu kama vile maji, shule, hospitali, barabara, umeme, ulinzi na Taasisi za utoaji haki. Ni muhimu sana na ninawaomba kwa dhati kabisa kushiriki kuhesabiwa. Na nitumie fursa hii kuwaomba kwa unyenyekevu kabisa viongozi wote wa dini zote mshiriki pamoja nasi na kutusaidia kuwahamasisha waumini wenu kushiriki zoezi hili muhimu kila mpatapo nafasi ya kuzungumza nao na kuwahudumia. Tusifiche idadi ya watoto au watu wenye ulemavu wa aina yeyote.

***Ndugu zangu***

Naomba nimalize maana tunahitaji pia muda wa kwenda kusherehekea siku hii nzuri na yenye baraka tele, lakini muda sio rafiki siku zote, natumaini Mungu atatupatia siku nyingine tena. Nawashukuru sana Wahashamu Maaskofu, Mapadri na waumini wenzangu kwa heshima kubwa mliyotupatia kama Serikali kushiriki nanyi baraka hizi. Nirudie tena kuwapongeza na kuwatakia Mapadri wapya utume mwema, wenye mafanikio na baraka tele. Naomba pia niwakabidhi zawadi ili iwe kumbukumbu ya siku hii muhimu ya leo iliyompendeza Bwana ninyi mpate Sakramenti ya Upadre.

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.**

**TUMSIFU YESU KRISTO!**